JINA:…………………………………..…. SHULE…………………………………………

NAMBARI YA MTAHINIWA…………..………TAREHE:………....SAHIHI…………..

102/2
KISWAHILI (Lugha)
KARATASI YA PILI
KIDATO CHA NNE
MUDA: 2½

# TATHMINI YA DAYOSISI YA KAKAMEGA
# MTIHANI WA JULAI/AGOSTI

**MAAGIZO**

a) Andika jina lako na nambari yako ya mtihani katika nafasi ulizoachiwa hapo juu
b) Jibu maswali yote
c) Majibu yote yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali
d) Watahiniwa lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo

## Kwa Matumizi ya Mtahini Pekee

| SWALI | UPEO | ALAMA |
|---|---|---|
| 1 | 15 | |
| 2 | 15 | |
| 3 | 40 | |
| 4 | 10 | |
| JUMLA | 80 | |

1. **UFAHAMU** (alama 15)

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali yanayofuata.

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yanayobadilika mno. Mtazamo wake maishani ni tofauti kabisa na ule wa wanawake walioishi karne za ishirini na kumi na tisa. Yeye hatarajii kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke wa bwana, kumzalia mumewe watoto na daima dawamu kuwa mwendani wa vijungu jikoni akiwapikia watoto wa bwanake chakula na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani kuchanja kuni, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumia nyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamana na mwanamume. Akanyagapo mume papo naye huutia wayo wake.

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanawake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika masomo ya lugha, historia, jiografia, hesabu, sayansi na mengineyo sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa huzifanya kazi zote. Kuna walimu, madaktari, wahandisi n ahata mabalozi. Mwanamke wa kileo si tena mama jikoni. Anataka apae angani, apigane vitani bila kusaza kushiriki katika uongozi wa mataifa yao. Wametokea wanawake waliotamalaki ulimwenguni mzima. Marehemu waziri mkuu wa Uingereza Margaret Thatcher ni miongoni mwa wanawake mashuhuri waliosifika katika ulimwengu huu.

Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake, iwapo ni mfanyi biashara, imepiga hatua ya kutomrudisha ukatani.

Mwanamke wa kisasa haamuliwi jambo lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kuna upande mwingine, mwanamume wa kisasa, ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume, hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akitamanai ya kale lakini wapi! Analazimika kumkubali mwanamke huyu kama mshirika sawa maishani, na kuishi naye, apende asipende. Shingo upande analazimika kukubali kwamba mabadiliko haya sio mithili ya kiwingu kipitacho, bali ni aushi.

a) Msemo ‘mwendani wa vijungu jiko’ unadhihirisha hali gani ya mwanamke katika jamii? (alama 2)

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

b) Jamii inafanya mwanamke kuwa hayawani wa mzigo. Fafanua (alama 2)

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

c) Eleza maana ya **akanyagapo mume. Naye papo huutia wayo wake**. (alama 1)

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

d) Tofauti zipi za kimsingi zilizopo baina ya mwanamke wa kisasa na wa zamani? (alama 3)

..................................................................................................................

..................................................................................................................

..................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

e) Mwanamume wa kisasa anamwonaje mwanamke wa kisasa? (alama 1)

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

f) Taja mifano mitatu ya mawazo ya kihafidhina kama yanavyojitokeza makalani. (alama 3)

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

.......................................................................................................................

g) Eleza maana ya: (alama 3)

i. Tamalaki

.......................................................................................................

.......................................................................................................

.......................................................................................................

ii. Ukatani

.......................................................................................................

.......................................................................................................

.......................................................................................................

iii. Taasubi za kiume

.......................................................................................................

.......................................................................................................

.......................................................................................................

**2. UFUPISHO**

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Ukame ni tukio hatari la kimaumbile. Athari zake hutofautiana kutoka eneo moja hadi lingine. Kwa sababu hiyo, si rahisi kuelewa dhana ya ukame; kwa hakika si rahisi kuifafanua dhana hii. Katika eneo la Bali, kwa mfano, isiponyesha kwa muda wa siku sita wenyeji huchukulia hali hiyo kuwa ukame japo kiasi hicho cha mvua ni kikubwa mno ikilinganishwa na Libya ambayo hupata kiasi kidogo cha chini ya milimita 180 ya mvua kwa mwaka.

Katika hali ya kawaida ukame hutokana na kipindi kirefu cha uhaba wa mvua hasa katika mwaka mzima au zaidi. Uhaba huu wa mvua huweza kusababisha uhaba wa maji kwa shughuli, kundi au sekta Fulani. Shughuli za binadamu huweza kufanya hali ya ukame kuwa mbaya zaidi. Shughuli hizo ni pamoja na kilimo, unyunyiziaji maji na ukataji wa miti.

Ni vigumu kubaini wakati mahususi ambao ukame huanza kwani kipindi hicho cha ukosefu wa mvua huwa cha mfululizo, nae neo huendelea kupata mvua iliyopungua kwa miezi au hata miaka. Mimea hukauka na wanyama hufa kutokana na ukosefu wa maji. Ukame basi huwa tayari kwa maisha ya binadamu na viumbe wengine kwa kuwa huweza kusababisha njaa na kuyafanya maeneo kuwa majangwa.

Mbali na ukosefu wa mvua, ukame pia husababishwa na kiangazi. Kiangazi huongeza kiwango cha joto. Joto hilo hufanya maji yaliyohifadhiwa kuwa mvuke haraka, hivyo kiwango chake kupungua. Hali ya *el ninyo* pia husababisha ukame katika baadhi ya maeneo ambayo huwa hayana mvua. Upepo huivutia mvua mahali panaponyesha na kuliacha kame eneo ambalo halina mvua ya aina hii. Hata katika maeneo yenye mvua ya *el ninyo,* kiangazi kikali huifuata na hivyo kusababisha ukame. Hali hii huitwa *la nina.* Mambo yanayotokana na mabadiliko ya hali ya anga ulimwenguni pia yanaweza kuchangia kuwepo ukame. Ongezeko la joto duniani linafanya hali ya ukame kuwa mbaya Zaidi.

Ukame una madhara chungu nzima kwa binadamu. Madhara hayo huweza kuwa ya kiuchumi, kimazingira au hata kijamii. Ukame husababisha kupungua kwa mimea na mavuno. Huweza pia kutokea dhoruba za mchanga. Dhoruba hizi hutokea palipo na jangwa. Ukosefu wa maji ya kunyunyizia mimea husababisha njaa na magonjwa kama vile utapiamlo yanayotokana na ukosefu wa lishe bora. Makazi ya wanyama wa nchi kavu na wale wa majini pia huathiriwa vibaya. Hali kadhalika, ukame husababisha uhamaji. Hii inamaanisha kuwa jamii huweza kutoka katika makazi asilia na wakati mwingine huweza hata kuwa wakimbizi.

Ukame husababisha ukosefu mkubwa wa maji. Ukosefu huu huwa na athari hasi kwa maendeleo ya viwanda kwa kuwa vingi huhitaji kiasi kikubwa cha maji. Juu ya hayo, maji huhitajika katika kuzalisha umeme. Umeme una matumizi mengi katika viwanda, nyumbani, afisini na hata hospitalini. Ukosefu wa umeme basi huwa ni tatizo kuu.

Aidha, ukame husababisha madhara mengi, binadamu wanaweza kujikinga kutokana na uhaba wa rasilimali za asili kama vile chakula na maji. Pia mioto mikubwa huweza kuenea haraka wakati wa ukame na hivyo kusababisha vifo vya binadamu na wanyama na uharibifu wa rasilimali nyingine.

Ingawa ukame husababisha madhara mengi, binadamu wanaweza kujikinga kutokana nao kwa kupunguza makali ya ukame. Jambo la kwanza wanaloweza kufanya binadamu ni kuhifadhi maji. Maji ya mvua yanafaa kuhifadhiwa katika mabwawa na mapipa. Haya yanaweza kutumiwa wakati wa ukame hasa katika kukuza mimea. Mkakati mwingine ni kutumia mbinu za kupunguza chumvi na kemikali nyingine zilizomo kwenye maji ya bahari ili yaweze kutumika katika unyunyiziaji wa mimea. Hili litapunguza tatizo la ukosefu wa chakula. Pia ni muhimu kufanya utafiti kuhusu hali ya anga ili kupanga na kuweka mikakati ifaayo kukabiliana na hali hiyo.

Ni muhimu kuwa na mipangilio mizuri ya matumizi ya ardhi. Mathalani upanzi wa mimea itakayozuia mmomonyoko wa udongo, kubadili aina ya mimea inayokuzwa sehemu fulani Pamoja na upanzi wa mimea isiyohitaji mvua nyingi ni hatua mwafaka. Aidha, ni vizuri kupunguza matumizi ya maji hasa katika mazingira ya nyumbani kwa mfano tunapofua na kuosha. Njia nyingine ya kukabiliana na tatizo hili ni kusafisha maji yaliyotumiwa ili kuyatumia tena.

a) Kwa maneno **50**, eleza visababishi vya ukame kwa mujibu wa taarifa.

(alama 4; 1 mtiririko)

Matayarisho

..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................

Nakala safi

..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................
..............................................................................................................................

b) Fupisha ujumbe wa aya ya **tano** hadi **saba** kwa maneno 70. (alama 6; 1 mtiririko)

Matayarisho

Nakala safi

c) Eleza masuala ambayo mwandishi ameibua katika aya mbili za mwisho kwa maneno **60.** (alama 5; 1 mtiririko)

Matayarisho

Nakala safi

................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................

3. **MATUMIZI YA LUGHA** (alama 40)

a) Andika neno lenye muundo ufuatao. (alama 2)
Kipasuo ghuna cha midomo, irabu ya kati mbele, kipasuo hafifu cha ufizi, irabu ya juu mbele.
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................

b) Weka shadda kwenye neno ALA ili kutoa maana mbili tofauti. (alama 2)
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................

c) Tasfidi sentensi kwa wakati ujao hali timilifu. (alama 2)
Mama alizaa msichana.
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................

d) Tunga sentensi ukitumia vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizoko mabanoni.

i. Chota (tendesha) (alama 2)
................................................................................................................................
................................................................................................................................

ii. Fa (tendea) (alama 2)
................................................................................................................................
................................................................................................................................

e) Ainisha mofimu katika neno lifuatalo: KATIKA (Kitenzi) (alama 3)
................................................................................................................................
................................................................................................................................
................................................................................................................................

f) Unda nomino mojamoja kwa kila kitenzi. (alama 2)

i. Shuku
................................................................................................................................
................................................................................................................................

ii. Kwea

g) Eleza matumizi ya kiambishi 'O' katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Waliopita mtihani walifanya marudio vizuri.

h) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia matawi. (alama 4)

Wanafunzi wengi walipita mtihani ulioandaliwa.

i) Toa mfano mmoja wa neno lenye muundo wa silabi ufuatao KIK (alama 1)

j) Andika katika ukubwa wingi. (alama 2)

Meza ilikarabatiwa kwa nyundo ile

k) Mwadime alinunua simutamba mpya kwa shilingi elfu kumi na kumtuza mwanafunzi bora.

(Anza sentensi kwa shamirisho kitondo) (alama 3)

l) Onyesha miundo yoyote miwili ya majina ya ngeli ya LI-YA. (alama 2)

m) Tambua aina za virai katika sentensi ifuatayo. (alama 3)

Aisee! Yale mawimbi ya tsunami yaliangamiza biashara nyingi.

n) Tunga sentensi moja kudhihirisha maana mbili ya neno BUNDA. (alama 2)

o) Andika sentensi ifuatayo katika usemi halisi. (alama 3)

Kibibi alisema kuwa kile kiguu cha kijibwa cheusi siku hiyo kingekuwa marufuku kwake.

p) Tambua maana mbili ya sentensi ifuatayo: Waite wale (alama 2)

q) Eleza matumizi matatu ya kibainishi. (alama 3)

## 4. ISIMUJAMII

a) Eleza sifa nne za lugha ambayo wewe kama nyapara wa kiwanda cha kuoka mikate cha matopeni utatumia ukiwahutubia walio chini yako. (alama 4)

b) Taja lahaja zozote tatu za Kiswahili zinazozungumzwa Pwani mwa Kenya. (alama 3)

c) Dhibitisha kuwa Kiswahili ni lugha ya Kibantu. (alama 3)